Migogoro ya ndoa, malezi ya kambo na kuasili watoto vyashika kasi nchini UK. 3



Prof. Janabi aanzisha vita kukabili milipuko ya magonjwa kwa bajeti ya Afrika UK. 4




# Nipashe

Jumanne Desemba 23, 2025 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0582259

epaper.ippmedia.com / www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII



Guardian

GAZETI BORA TANZANIA

SUPERBRAND MARA 11 MFULULIZO



URITHI WA UBORA, NA SAFARI YA MAFANIKIO


## DOROTHY SEMU:

# Serikali Umoja Kitaifa imepoteza mwelekeo



**Avunja ukimya kinachoendelea Zanzibar na hatima ya ACT-Wazalendo, vigingi vya upinzani... CCM yamjibu papo kwa hapo...**

"Bila makubaliano ya msingi katika masuala hayo, SUK inabaki kuwa jina tu. Tukishakubaliana kwenye haki, uchaguzi wa kweli na uwajibikaji, ndipo tutakuwa na mazingira ya kufanya uamuzi wenye maana juu ya ushiriki wetu," | Dorothy Semu

HABARI UK. 5



Mbeto Khamis Mbeto

## Krismasi kuwa chini ya ulinzi maalumu kuanzia ibada hadi ulingo wa starehe

JESHI la Polisi Tanzania limethibitisha kuwa hali ya usalama nchini imebaki shwari kwa kipindi cha takribani siku 10 zilizopita, licha ya kutokea kwa matukio machache ambayo yameshughulikiwa kwa mujibu wa sheria za nchi na mikataba ya kikanda na kimataifa...



Uk. 2,3

# Mwamko tiketi za usafiri mtandaoni bado tatizo






Abiria wanaosafiri kutoka Dar es Salaam kwenda mikoani wakiwa katika Kituo cha Mabasi cha Magufuli kilichoko Mbezi jana. PICHA: IMANI NATHANIEL

HABARI UK. 2

## Ubakaji wanawake na watoto tishio Zanzibar



MATUKIO 107 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa visiwani hapa kwa mwezi uliopita ikiwa ni ongezeko la asilimia 8.1 ikilinganishwa na 99 ya Oktoba mwaka huu, idadi kubwa ikiwa ni ya ubakaji wanawake na watoto. Mtakwimu Ahamad Hassan Suleiman, alitoa takwimu hizo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari...

HABARI UK 17

CamScanner

HABARI KITAIFA

RIPOTI

# Mwamko tiketi za usafiri mtandaoni bado tatizo

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imesema kuwa asilimia 11 ya abiria wanaosafiri kwa mabasi wanakata tiketi mtandaoni, huku asilimia 89 wakibaki kutumia mfumo wa zamani wa fedha taslimu.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, Dk. Habibu Suluo, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu ukaguzi wa usafiri uliofanyika katika mikoa mbalimbali nchini.

Dk. Suluo alisisitiza umuhimu wa wamiliki wa mabasi kuanzisha mfumo wa malipo mtandaoni. "Tunawasihi wamiliki kuhakikisha malipo yanafanyika mtandaoni ili waweze kufuatilia miamala, idadi ya abiria na usalama wa fedha," alisema.

Vilevile, Dk. Suluo alitoa wito kwa abiria kutumia njia ya mtandao katika kununua tiketi, akibainisha kuwa ni salama, huzuia kupandishwa kwa nauli bila taarifa na huingiza majina kamili kwenye mfumo wa tiketi.

"Kama unaweza kutuma fedha kwa ndugu yako mtandaoni, kwa nini usikate tiketi kwa njia hiyo?" aliuliza.

> **"Kama unaweza kutuma fedha kwa ndugu yako mtandaoni, kwa nini usikate tiketi kwa njia hiyo?"**


Katika kipindi hiki cha mwisho wa mwaka, LATRA imetoa vibali 252 vya muda ili kusaidia usafiri wa abiria kwenda kwenye mapumziko ya sikukuu za mwisho wa mwaka. Vibali hivi vimetolewa kupitia ofisi za LATRA mikoa mbalimbali.

Dk. Suluo pia alibainisha kuwa kutoka Desemba 8 hadi 20, jumla ya magari 4,805 yamekaguliwa, huku makosa 515 yakiwamo kutotumia tiketi za kielektroniki, kutokuzingatia masharti ya leseni na kutotumia mfumo wa ufuatiliaji magari (i-button).

"Kwa ujumla hali ni shwari, hakuna matukio mabaya. Tutaendelea na ukaguzi ili kuhakikisha usafiri salama," alisema.

Aidha, mamlaka hiyo imeongeza ulinzi na ukaguzi kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi, kuhakikisha usalama na ubora wa usafiri katika mikoa yote.

Dk. Suluo aliwataka wananchi kufuata masharti yote ya usafiri, kutumia malipo ya mtandao na kushirikiana na mamlaka ili sikukuu za mwisho wa mwaka zipite kwa amani na usalama.



Abiria wanaosafiri kutoka Dar es Salaam kwenda mikoani wakiwa katika kituo cha mabasi cha Magufuli kilichopo Mbezi jana. **PICHA IMANI NATHANIEL**

Guardian VOTED Superbrands EAST AFRICA'S CHOICE 2024-2026

# The Guardian

www.ippmedia.com

epaper.ippmedia.com 30 YEARS Anniversary Guardian www.ippmedia.com

@TheguardianTz01 theguardianltd epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com feedback@guardian.co.tz LIKE & FOLLOW US

ISSN 0856 - 5434 ISSUE No. 9665 • PRICE: Tsh 1,000, Kenya sh100 TANZANIA TUESDAY 23 DECEMBER, 2025




'Utilise weather data in planting' Page 2



Govt warns job seekers Page 3




Legal procedures for eligible families Page 4



Prepaid meters to boost revenue Page 5

# 'Bus passengers still pay cash despite digital push'

By Getrude Mbago

ONLY 11 percent of bus passengers currently purchase tickets online, with the bulk 89 percent paying in cash, the Land Transport Regulatory Authority (LATRA) has indicated.

Dr. Habibu Suluo, the LATRA director general, made this observation while inspecting transport operations in Arusha and Kilimanjaro regions over the weekend, saying the situation denies the government substantial revenues and undercuts passenger rights.

This traditional payment method persists despite major government investments in digital ticketing systems and a range of compliance measures, he said, noting that the slow adoption of digital payment systems "leaves room for financial mismanagement and limits oversight of passenger flows."

"Online payments make it easier for bus operators to monitor revenue, track the number of passengers and reduce fare complaints. Yet, the vast majority of travellers still rely on cash payments, which are vulnerable to misreporting," he said.

The government has for some years made concerted efforts to modernize ticketing in the public transport sector, introducing online ticketing platforms for long-distance buses to reduce fare manipulation and improve transparency, he stated.

Compliance measures at major bus terminals, requiring operators to integrate online ticketing systems into their operations were initiated, requiring that bus owners and operators fully adopt online ticketing. Doing

TURN TO PAGE



Minerals minister Anthony Mavunde (gesturing) pictured yesterday while on inspection tour of a site in Mwendakulima ward in Kahama municipality previously used by the since-closed Buzwagi Mine but now filled with rainwater. Photo: Correspondent Shaban Njia

USAFIRI



Abiria wakiwa stendi ya mabasi Moshi mjini wakisubiri usafiri wa kuelekea Rombo mkoani Kilimanjaro. Picha Ombeni Mjema

# Ukame wa abiria wakatika vituoni

Janeth Joseph na Devotha Kihwelo, Mwananchi
mwananchipapers@mwananchi.co.tz

**Moshi/Dar.** Hali Hali ya ukame wa abiria uliokuwa ukionekana katika Kituo Kikuu cha Mabasi cha Magufuli katika siku za hivi karibuni imebadilika baada ya ongezeko la wasafiri kuelekea sikukuu za Krismasi na Mwaka mpya.

Kutokana na hali hiyo, Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (Latra) imetoa vibali vya muda kwa ajili ya kusaidia kuongeza upatikanaji wa usafiri, huku Shirika la Reli Tanzania (TRC) likiongeza treni moja ya abiria.

**Mil 1.9**
Idadi ya tiketi zilizouzwa kati ya Desemba mosi hadi Desemba 20 mwaka huu.

**Sh71 bil**
Jumla ya nauli iliyolipwa na abiria tofauti katika kipindi hicho.

### Hali ilivyo Dar es Salaam

Jijini Dar es Salaam, siku chache kabla ya Krismasi, hali ya usafiri katika kituo cha Magufuli ilielezwa kuwa nzuri, licha ya mabasi mengi yanayoelekea mikoa ya Kaskazini kuondoka yakiwa yamejaa abiria.

Mmiliki wa mabasi ya RN Express, Nelson Kimaro aliema tangu Desemba 21, kumekuwa na ongezeko kubwa la abiria, hali inayofanya upatikanaji wa mabasi kuwa mgumu katika baadhi ya safari.

"Ukifika stendi ukaulizia gari la kwenda Arusha au Kilimanjaro, utakuta mengi yamejaa," alisema.

Alisema hali hiyo ni tofauti na ilivyokuwa kati ya Desemba 10 na 19, kulikuwa na uhaba wa abiria uliosababisha biashara ya usafiri kuwa ngumu.

"Mabasi yalikuwa yanaondoka na abiria 20 au 30 tu. Kipindi hicho ndipo nauli zilikuwa zinashuka," amesema.

Kwa mujibu wa Kimaro, kwa sasa nauli zimebaki katika viwango vya kawaida, zikianzia Sh42,000 kwa mabasi ya kawaida na kufikia Sh60,000 kwa mabasi ya daraja la VIP, kutegemeana na aina ya huduma.

Hata hivyo, katika kukabiliana na changamoto ya usafiri, Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (Latra) imesema hadi Desemba 20, ilitoa vibali 252 vya muda kwa ajili ya kusaidia kuongeza upatikanaji wa usafiri.

Mkurugenzi Mkuu wa Latra, Habibu Suluo amesema kati ya Desemba mosi na Desemba 20, jumla ya tiketi milioni 1.978 ziliuzwa, huku nauli zilizolipwa zikifikia Sh71.347 bilioni.

Hata hivyo, changamoto bado zinaendelea kuwepo. Dereva wa gari la 'special hire', Shaaban Nguruka, alisema kuanzia Desemba 20 wanapata abiria wengi, hususan wanaoelekea mikoa ya Kaskazini.

Alisema nauli kwa safari hizo hufikia hadi Sh55,000, akieleza kuwa hulazimika kufidia gharama za safari ya kurudi ambayo mara nyingi huwa na abiria wachache.

### TRC yaongeza nguvu

Akizungumza na *Mwananchi* jana, kuhusu hatua zilizochukuliwa na TRC, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano cha shirika hilo, Fredy Mwanjala alisema ongezeko la mahitaji ya usafiri kuelekea sikukuu hizo limewalazimu kuongeza treni moja ya abiria kutoka Dar es Salaam kuelekea mikoa ya Kaskazini.

Alisema kwa upande wa reli ya kisasa (MGR), ratiba ya kawaida ya safari za kuelekea Arusha na Moshi ni kila Jumatatu na Ijumaa, na treni huondoka saa nane mchana.

Hata hivyo, kuanzia sasa hadi Januari mwakani, alisema TRC imeongeza treni nyingine itakayokuwa ikifanya safari kila Jumamosi.

"Tumelazimika kuongeza treni moja nzima ambayo itakuwa inaondoka saa nane mchana kila Jumamosi hadi Januari 2026. Lengo ni kuhakikisha tunawahudumia Watanzania wanaosafiri kwenda mikoa ya Kaskazini kwa ajili ya sherehe za Krismasi na Mwaka mpya bila shida," alisema Mwanjala.

Aliongeza kuwa uamuzi huo umezingatia makundi mbalimbali ya wasafiri, wakiwamo watumishi wa umma na wanafunzi wanaosafiri wakati wa likizo na kurejea kazini au shuleni ifikapo Januari.

Kwa upande wa reli ya kati inayounganisha Dar es Salaam na Kigoma, Mwanjala alisema TRC imeongeza idadi ya mabehewa kutoka 16 ya kawaida hadi 20, baada ya kukarabati mabehewa manne ya ziada.

"Katika kipindi hiki cha kuelekea sikukuu za Krismasi na Mwaka mpya, tutatumia mabehewa 20 badala ya 16. Hatua hii inalenga kubeba abiria wengi zaidi na kupunguza msongamano," alisema.

**"Tumelazimika kuongeza treni moja nzima ambayo itakuwa inaondoka saa nane mchana kila Jumamosi hadi Januari 2026. Lengo ni kuhakikisha tunawahudumia Watanzania wanaosafiri kwenda mikoa ya Kaskazini kwa ajili ya sherehe za Krismasi na Mwaka mpya bila shida."**

Fredy Mwanjala, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano TRC

### Moshi yafurika

Hali ya msongamano wa watu na magari imeonekana pia katika Mkoa wa Kilimanjaro, hususan katika Manispaa ya Moshi.

Uchunguzi wa *Mwananchi* ulibaini katika nyakati za mchana na jioni, maeneo ya katikati ya mji wa Moshi kumekuwa na msongamano mkubwa wa watu na magari hali inayosababisha foleni ndefu barabarani.

Mkazi wa Moshi, Ebenezer Swai akizungumzia hilo alisema hali hiyo ni ya kawaida kila unapofika msimu wa sikukuu za mwisho wa mwaka.

"Kipindi hiki, mji wa Moshi hufurika watu. Magari ni mengi, watu pia ni wengi, na wengine wanaegesha magari barabarani kwa sababu hakuna maeneo ya kutosha," alisema.

Kwa upande wa usafiri wa ndani, abiria anayesafiri kutoka Moshi kwenda Wilaya ya Rombo, Anna Shayo alisema ongezeko la watu limesababisha magari mengi kujaa mapema, hivyo abiria kulazimika kusubiri kwa muda mrefu. "Magari ni machache na watu ni wengi, wakati mwingine tunasubiri gari kwa muda mrefu kabla ya kupata nafasi," alisema.



Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (Latra), Habibu Suluo mwenye kofia nyeusi akizungumza na abiria katika operesheni ya ukaguzi wa vyombo vya usafiri unaoendelea nchini

CamScanner

# Muungwana Lazima Nilonge



Jumanne Desemba 23, 2025 (19) Nipashe

## LATRA mko wapi abiria tunaonewa?

Faustine Feliciane

HILI nalo si la kufumba macho wala kulikalia kimya katika baadhi ya daladala baada ya kuzuka mtindo wa makonda kutangazia abiria kuwa kama hawana nauli kamili hakuna chenji ya kurudisha.

Kwani jambo hili limekuwa likizua malumbano yasiyokuwa ya lazima katika vyombo hivyo vya usafiri baada ya kondakta kugoma kurudisha chenji kutokana na vitendo hivyo kuonesha kumuudhisha abiria kwa kudai haki yake hiyo ya msingi.

Vitendo hivyo ambavyo ni sawa na unyonyaji, kujipatia fedha kwa njia za udanganyifu, unyang'anyi na wizi wa kuaminiwa, vilikuwa vimeanza taratibu na sasa vimedhibitika kushika kasi na kusambaa hadi kwa waendesha bajaji na bodaboda kwa kumkatalia abiria kuwa walitangaza tangu safari ikianza kuwa nauli kamili iwe kwa hiki la-sivyo atafute usafiri mwingine.

Ni hivi karibuni katika bajaji safari ikianza kituo cha Tabata Kimanga Dar es Salaam, akiteremsha abiria External kwa nauli ya Sh 700, kila abiria aliyempa Shilingi 1,000, alimpatia Shilingi 100 huku akitamba kwa kuwaambia waende kokote kule hawezi kurejesha chenji kamili kwa sababu aliwatangazia kabla ya kuanza safari kila mmoja awe na nauli kamili yaani Shilingi 700.

Kauli hiyo ilisababisha malumbano baina yake na mmoja wa abiria hao huku akitishia kuwa amemkariri sura na kumpiga marufuku kupanda bajaji yake popote atakapoikuta iwe kituoni Kimanga au External.

Kana kwamba haitoshi, dereva huyo aliteremka kwenye bajaji huku amkisisitiza abiria yule kuwa yeye haogopi vyombo vya ulinzi na usalama wala mamlaka aliyopewa jukumu la kusimamia usafirishaji abiria, iwe ardhini, majini, angani na kumtaka anakili namba ya chombo chake usafiri na kupeleka kokote kule, hababaiki.

Baadhi ya madereva waliokuwa katika kituo hicho cha External, walionesha kukerwa na kitendo cha mwenzao huyo na kuamua

> **Kauli hiyo ilisababisha malumbano baina yake na mmoja wa abiria hao huku akitishia kuwa amemkariri sura na kumpiga marufuku kupanda bajaji yake popote atakapoikuta iwe kituoni Kimanga au External.**

kurejesha chenji kwa abiria huyo kwa kuwa alikuwa amepanga kuongeza kiasi hicho cha Shilingi 400 apate nauli ya kuendelea na safari yake kwa Shilingi 500 hadi kituo cha daladala Mwenge.

Baadaye tena jioni, abiria waliokuwa katika daladala linalofanya safari zake kati ya Mwenge na Pugu, kondakta wake alisikika akiwatangazia abiria wa kituo cha River Side kuwa, hatakuwa na Shilingi 100 ya kurudisha chenji atakayempa Shilingi 600 ambazo ni 200 tatu, ili kulipa nauli ya Shilingi mia tano.

Kama alivyozoeleka, ndivyo alivyoendelea kwa kujiwekea kiasi hicho cha fedha na kuwa malalamiko kwa baadhi ya wazee, vijana na wanawake waliokuwa wakitoka kwenye shughuli zao za kujipatia kipato.

Muungwana lazima nilonge kuwa, vitendo hivyo ni kosa la jinai na athari zake ni kusababisha kuvunjika kwa amani na utulivu na kuzusha vurugu hata kuhatarisha maisha yao kutokana na kuvumilika kwa vitisho, unyanyasaji na udhalilishaji kutoka kwa madereva na makondakta daladala.

Mwanzoni vitendo hivyo vilidaiwa kutokea katika daladala zinazofanya safari zake kutoka pembezoni hadi katika ya Dar es Salaam na sasa vinakithiri kwa kusambaa katika njia nyingine.

Kimsingi, askari hususani wa kikosi cha usalama barabarani wako katika barabara mbalimbali kuhakikisha sheria zinafuatwa kwa manufaa ya wananchi wanaotumia vyombo vya usafiri iwe wa daladala, bajaji, bodaboda, mabasi ya masafa marefu na magari binafsi.

Kwa msisitizo, Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA) iko kwa ajili ya kuhakikisha haki ya abiria inalindwa na ndio sababu imetoa namba zake kwa kupandikwa kwenye kila daladala.

LATRA imetoa namba maalumu kwa abiria kupiga simu na kutoa taarifa kutokana na ukiukwaji sheria na haki za binadamu unaofanywa na makondakta wa daladala ili hatua kali zichukuliwe dhidi ya muhusika.

LATRA ingieni kwenye magari mnatangamane na abiria mjue shida zao na kuwachukulia hatua wahalifu.

Jamhuri Jumanne Desemba 23/2025 Pg 9



# Latra: Nauli ya Sh 1,000 ni ya mpito

**DAR ES SALAAM**

NA MWAANDISHI **WETU**

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA), Habibu Suluo (pichani), amesema nauli ya Sh 1,000 inayotumika katika mabasi yaendayo haraka ni ya mpito.

Saluo amewaambia waandishi wa habari jijini Arusha mwishoni mwa wiki wakati akitoa ufafanuzi kuhusu kiwango hicho cha nauli hiyo ambayo imeonekana kulalamikiwa na baadhi ya watumiaji wa usafiri huo jijini Dar es Salaam.

Amesema nauli inayotumika sasa iliridhiwa kuwa Sh 1,000 kwa tangazo la Serikali la Agosti 29, mwaka huu na pande zote mbili.

Amesema nauli hiyo, ni ya mpito wakati Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART), ukiendelea kukusanya maoni ya wadau ili kuja na nauli ya kudumu kama ilivyokuwa mwanzo.

Amesema kiwango cha mpito kimewekwa ili kuwavutia wawekezaji kuja kuwekeza Tanzania, akisema kinyume chake itakuwa viguma watu kuja kufanya biashara nchini kutokana na mazingira kutolipa.

Amesema kiwango hicho cha nauli hakihusiani na matukio ya Oktoba 29, mwaka huu, bali matukio ya siku hiyo yulisababisha uharibifu wa miundombinu.

"Ni kwamba imezoeleka Latra ndiyo hutangaza nauli, Dart walitangaza na sisi tukaridhia, na tangazo likachapishwa kwenye Gazeti la Serikali," amesema.

Mtendaji Mkuu wa Dart, Said Tunda, amesema nauli hiyo ndiyo kiwango kinachoweza kumvutia mwekezaji , huku mabasi yakiendeshwa na sekta binafsi.

"Tupo kwenye mstari, kwa sababu nia si kuwaumiza wananchi, baada ya huduma kusimama, watu walikuwa wakilipa kati ya Sh 5,000 hadi Sh 6,000 kwa safari ambayo sasa wanalipa shilingi 1,000," amesema.




**Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA), Profesa Ahmed Ame (kulia), akipokea tuzo ya mshindi wa kwanza kwa mwaka 2024/25 miongoni mwa taasisi zilizo chini ya Wizara ya Uchukuzi kutoka kwa Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Joseph Mkude.**

The citizen December 23, 2025 Tuesday Pg 5

# Latra: Only 20pc of bus passengers using online ticketing

By Hellen Nachilongo
@TheCitizenTz
hnachilongo@tz.nationmedia.com

**Dar es Salaam.** Passenger uptake of the online bus fare payment system remains low, the Land Transport Regulatory Authority (Latra) has said, prompting renewed calls for travellers to use digital platforms to curb ticket touting and ensure fares paid are properly captured in the system.

Latra director general Habibu Suluo said that between December 1 and 20 this year, total fare collections amounted to Sh71 billion, of which nearly Sh8 billion was paid through online platforms, while about Sh63 billion was paid in cash.

"This means only about 20 per-cent of passengers are buying tickets online, while the majority still pay in cash," Dr Suluo said.

He encouraged passengers to adopt online ticket purchases to prevent overcharging and to guarantee accurate fare payment.

"If you can send money to a relative through your phone, why not buy your ticket online? This ensures you pay the correct fare and are not overcharged," he said.

Dr Suluo also called on bus owners to ensure payments are made through electronic systems so that revenues can be properly monitored by the regulator.

He added that online ticketing captures passengers' full details in the system, enhancing accountability and security in public transport operations.

Dr Suluo said Latra conducted a nationwide inspection exercise from December 8 to 22, during which 4,405 vehicles were inspected, most of them at the Mikese inspection station. The exercise, he said, was part of joint efforts with road safety stakeholders to support the government's drive to reduce road accidents and ensure safe travel, particularly during the busy festive season.

"This is a critical period when all stakeholders must work together to reduce road accidents and ensure citizens travel safely to meet their loved ones," he said.

According to Dr Suluo, Latra has intensified inspections across the country to ensure the availability of safe and reliable transport services amid high travel demand.

Inspection centres have been established nationwide to verify compliance with licence conditions and assess the quality of services offered to the public. "From these inspections, we identified 349 offences. The most common violations include failure to issue electronic tickets, non-compliance with licence conditions and some drivers operating without i-buttons," he said.

CamScanner